# KIBABII UNIVERSITY

## UNIVERSITY EXAMINATIONS

**2020/2021 ACADEMIC YEAR**
**FOURTH YEAR SECOND SEMESTER**

**SPECIAL/SUPPLEMENTARY EXAMINATION**

**FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)**

**COURSE CODE: KIS 405**

**COURSE TITLE: EDITODIAL METHODS IN KISWAHILI**

**DATE: 12-01-2022** **TIME: 2:00PM-4:00PM**

---

MAELEKEZO

Jibu maswali **matatu** pekee.

Swali la Kwanza ni la **lazima**

**MUDA: Masaa Mawili (2)**

**KIBU** observes **ZERO** tolerance to examinations cheating

**Maswali**

1. a). Harirri kifungu kifuatacho kwa kutumia alama za uhariri. (alama 10)

Kuna kisasili kilichokita miongoni mwa Wakenya wengi hasa wapangaji wa lugha kwamba kwambamatumizi ya lugha za kiasili ni ya kikabila, ya kutenganisha na kurudisha nyuma maendeleo (Luochna Ogutu, 2002). Hata hivyo, tunapotathmini vita vya kikabila nchini Kenya vya 1992 na disemba 2007 hadi Februari 2008, tunaona kwamba madai ya vita hivyo kusababishwa na tofauti za lugha hayana mashiko. wanasiasa wamekuwa wakiwachochea WAKENYA kwa misingi ya kikabila ili kufanya tofauti za kikabila zionekane kama msingi wa vita vya kikabila ilhali vita hivyo vilitokana hasa na katiba iliyokuwepo iliyompa rais mamlaka mengi kupita kiasi na matumizi mabaya ya hayo mamlaka (Roberts, 2009, Kriegler 2008 na Iraki, 2010).

Lugha hizi zimetumika katika nyimbo mbalimbali na kupendwa hata na watu wasio wazungumzaji wa lugha hizo. Kwa mfano kuna nyimbo kamavile *"Ategisi"* (na msanii Emmy Kosgei), "Jo Kristo Duto" (na kwaya ya St. Josephs Rapogi) na *"Umbolela Si"*(na msanii David Barasa) ambazo zinasikizwa na watu wengi wakiwemo hata wasio wazungumzaji wa lugha hizo. Kutokana na hali hiyo, ni bayana kwamba lugha hizo si mbaya ila matumizi mabaya ndiyo yanayofaa kushutumiwa.

Akisisitiza umuhimu wa lugha za kiasili, Mugambi (2007) anahoji:

> "Miradi ya kisasa inayokusudiwa kuelimisha umma nchini Kenya haiwezi kueleweka katika lugha nyingine yeyote isipokuwa lugha ya wananchi hao wa vijijini, ambao wengi wao hawajui kusoma wala kuandika" (Mugambi, 2007: 67).

Kusoma na kuandika anakorejelea msomi huyu ni kwa lugha za kigeni ambazo hasa ndizo lugha zinazotumika katika mfumo wa elimu. Miradi hii ni pamoja na, kampeni za kuhamasisha umma kuhusu katiba ya elimu ya uraia, tohara ya wanawake, marekebisho ya mfumo                      wa elimu na utetezi wa haki za wanawake. Kwa mujibu wa Mugambi (2007), kutokana na hali hiyo, mashirika ya serikali na wadau wengine wanastahili kutumia lugha za kiasili au lugha za wenyeji vijijini kadiri wawezavyo, ikiwa wanataka kupata madokeo yenye manufaa.

b) Fasili istilahi zifutazo zinazotumika katika taaluma ya uhariri: (alama 6)

i. Dibaji
ii. Blabu
iii. Faharasa

c) Kwa kutumia mifano, bainisha mambo yoyote manne ambayo uhariri wa yaliyomo hushughulikia katika mswada. (alama 8)

d) Kwa kutumia mifano, fafanua majukumu matatu ya mapitio ya vitabu katika taaluma ya uhariri. (alama 6)

2. Kwa kutumia mifano, fafanua changamoto sita zinazokumba uchapishaji wa kazi za Kiswahili katika karne hii ya 21. (alama 20)

3. a) Kwa kutumia mifano, onyesha manufaa yoyote matano ya vielelezo katika taaluma ya uchapishaji. (alama 10)

   b) Fafanua aina zozote tano za vielelezo katika taaluma ya uchapishaji. (alama 10)

4. Kwa kutumia mifano, tofautisha uhariri wa muundo na ule wa yaliyomo. (alama 20)

5. Umealikwa kwa mahojiano ya kazi kama mhariri wa shirika jipya la uchapishaji. Kwa kutumia mifano, fafanulia jopo hilo la uajiri umuhimu wa ufahamu sheria za uchapishaji kwa mhariri. (alama 20)